

KUUDHIHIRISHA UWEPO WA MUNGU ALIYE HAI

Zaburi 139:5-6. “Umenizingiranyuma nambele, ukaniwekea mkono wako

Sikiliza kile nabii wa Mungu alichosema kuhusu hilo:

Ni wangapi wanajua kuna tofauti kati ya kuonekana/kutokea kwa Kristo na kuja kwa Kristo? Ni maneno mawili tofauti. sasa ni wakati wa kuonekana/kutokea, kule kuja kutakuwa karibuni. Yeye hutokea katikati yetu, akifanya kazi alizowahi kuzifanya mwanzoni, katika kanisa lake. sasa, wewe ni sehemu ya hilo kanisa, na kwa neema unaamini (Waefeso 2:8-9). mimi ni mshirika wa hilo kanisa (Waefeso 4:4-6).

Ndugu Branham aliendelea: sasa mimi sio mhubiri mnajua sio hivyo. Sina elimu ya kulifanya hilo jambo. saa nyingine najisikia kutopenda kusimama hapa mbele ya watu wa Mungu, ambao wameitwa kwenye hiyo huduma. kuna mitume, manabii, walimu, wachungaji na wainjilisti (Waefeso 4:11-13). Siyo wote ni mitume, siyo wote ni manabii, siyo wote ni waalimu, siyo wote ni wainjilisti (Korintho 12:29-30). nimesimama hapa.

Huduma yangu ni tofauti na huduma ya wachungaji au walimu. Mimi siyo. Na kama nikisema mambo kwa namna isiyo sahihi, ndugu mnisamehe, simaanishi hivyo. lakini hii ndio huduma yangu kumdhahirisha, kwamba yupo hapa. [1]

Kwa ulinganisho. Musa akija akitokea uweponi pa Mungu akiwa na Neno la Mungu kwa wakati ule.... sasa, angalia, tukosasa katika kutoka 19. Usilikose hili sasa. Kutoka 19:20-21. Musa anakuja kutoka uweponi pa Mungu; amekaandani ya hilo neno. lile Neno lilikuwa limeandikwa, na alikuwa uweponi pa Mungu na lile neno, alikuwa na neno kwa ajili ya wakati ule. Kuna neno kwa kila wakati. Na Musa alikuwa anakuja, na uso wake uking'aa hivyo (Kutoka 34:34-35). (2Kor. 3:12-6). Lile Neno lilikuwa ndani yake, tayari kudhihirishwa, alitoe kwa watu.

Hiyo ilikuwa ni sheria tu; inabidi uende uangalie hiyo nakusema, usizini, usiibe, usiseme uongo, usifanye hivi, vile au vinginevyo” (Kutoka 20:1-17). inabidi uangalie hilo

Lakini hii ni Roho ambayo inakuja juu ya Neno lililoahidiwa kwa wakati huu, na unazaa na kujidhihirisha, siyo mawe mawili ya meza, ila uwepo wa Mungu aliye hai; siyo wazo Fulani la kuwazia alilolifanya mtu Fulani au triki ya haudini, lakini ni ahadi hasa ya Mungu ikifunuliwa na kufanywa iwe dhahiri hasa mbele zetu. Itakuwa ni aina ya pazia gani nyuma?

Na itakuja hutukia katika siku za mwisho, asema Mungu.. (Zakaria 14:6-7) unaona mahali tulipo. Ile nuru juu ya neno.... kadiri ya nuru ya jua inavyobadilika ile mbegu kutoka utukufu hadi utukufu (2Kor. 3:17-18). Sisi pia tunakuwa zaidi kama Yeye kadiri tunavyoishi uweponi pake; kama yeye. Tukifananishwa na sura yake iliyobarikiwa kama vile tutembeapo naye (Warumi 8:28-29). [2]

Na mpaka uje nyuma ya ngozi ya pomboo (Kutoka 36:19) mpaka utoke nje ya ngozi yako ya zamani, mawazo yako ya zamani. kanuni zako za zamani, Na uje katika uwepo wa Mungu; hapo sasa Neno linakuwa ni uhalisi unaoishi kwako; halafu unaamshwa kwenye utukufu wa shekina. Halafu Biblia inakuwa kitabu kipya; hapo sasa Yesu Kristo ni yule jana leo na hata milele. Unaishi katika uwepo wake. Ukila mkate wa wonyesho ambaye katika siku ile uliliwa na waaminio tu makuhani tu (Lawi 24:5-9). Na tumakuhani, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu walio tofauti, watoa sadaka za kiroho kwa Mungu (1Petro 2:9-10) lakini inabidi uje ndani, nyuma ya pazia kumuona Mungu aliyefunuliwa; hilo ni neno lake likidhihirishwa. [3]

Sasa, wakati Musa alipokuja, asingeweza kuchukuwa ujumbe wa Nuhu. Wala Nuhu asingeweza ujumbe wa Musa. Wala Joshua asingeweza kuuchukuwa ujumbe wao. Isaya asingeweza kuuchukuwa ujumbe mwingine. kila ujumbe ni kwa wakati ule. Na ukichukuwa wakati tunaishi ndani yake, wakati lile neno linatafsiriwa. Mungu analizungumza lile Neno na kulitengeneza Neno la wakati liishi. akitoa tafsiri yake. huyo ni Mungu ndani ya Kristo akijidhihirisha, kwa sababu Kristo ni neno. na wakati neno linapodhihirishwa hapo huyo ni Kristo katika kila wakati..

Hebu tuone kile neno linavyosema leo vile Yesu Kristo alivyo. Ni yeye yule jana, leo na hata milele, (Waebrania. 13:18). na njia pekee tuwezayo kujua yeye alicholeo ni kutafuta kile alichokuwa jana. Hapo sasa tunaona Yeye ni nani, angalia, lile neno lililotengwa/kusudiwa kwa ajili ya kila wakati, hilo neno linapodhihirishwa, huyo ni Kristo wa siku hiyo (Kolosa 1:26-28) kama tu ilivyokuwa katika kila moja ya hizi siku. [4]

Sasa kumbuka kuwa Kristo amefufuka kutoka kwa wafu na yuko miongoni mwetu. Na ulipata hilo uwepo wake ndani ya watu binafsi akiwa na uthibitisho wa yeye mwenyewe kujieleleza mwenyewe— neno lililo hai ambalo limeahidiwa kwa siku ya leo, likijieleleza kupitia wewe, uthibitisho wa ufunuo mkuu wa Mungu... angalia, ni kwa mtu binafsi tu, kamwe siyo kundi; ni binafsi, siyo katika kundi, utambulisho wake ni pamoja na mtu binafsi. Unalipata hilo? siyo na Wamethodist, siyo na Wabaptist, siyo na wapresbiterian, siyo na walutheri, siyo na Wapentekoste. Lakini kama mtu binafsi. “nitamchukuwa mmoja na kumuacha mmoja nitawalinganisha wao” Hiyo ni sawa. “kutakuwepo na wawili shambani; nachukuwa mmoja na

kumuacha mmoja. Kutakuwepo na wawili kitandani, na nitachukuwa mmoja na kumuacha mmoja (Luka 17:34-36).

Siyo kundi ni mtu binafsi uthibitisho wa mimba ya mtoto wa Mungu aliyejazwa na Roho Mtakatifu, akiwa amejisalimisha kabisa kwa Mungu ambapo hajali chochote kingine tena, na Roho Mtakatifu akiishi maisha yake, akionyesha uhai kupitia yeye, akionyesha uthibitisho wa kibinafsi wa Neno lenyewe likijieleleza kwa watu na kwa dunia [5]

Lile neno linakuwa hai katika miili yetu, ambalo linaonyesha uwepo wa Mungu [6]

Kristo anaishi siyo mimi ninayeishi, siyo mimi. Kristo anaishi ndani yangu. Siyo wewe unaishi, lakini Kristo anaishi ndani yako (Wagalatia 2:19-21). kwa sababu Yeye ni neno lililo hai ndani yako....[7]

Mungu alichagua katika siku za kutoka, aliita kundi na kutoka katika hilo kundi...nataka uone kitu Fulani, alipata wawili tu, ambao waliingia nchi ya ahadi Alichagua nini kuwachukuwa ilikuwatoa? Siasa? madhehebu? alichagua nabii akiwa na ishara na miujiza ya nguzo ya moto, ili kwamba watu wasije wakakosea (Hesabu14:13-14;Kutoka14:19-25).kile nabii alichosema ilikuwa ni kweli Mungu alishuka chini katika nguzo ua moto na kujithibitisha mwenyewe. kulionyesha neno lake hiyo ni sawa?

Hivyo ndivyo alivyoleta kutoka yake ya kwanza. Kutoka yake ya pili.....Mungu siku zote anaenda katika namba tatu ukamilifu wake ni utatu. kwanza, pili, na mvuto wa tatu na oh. Vyote. kila kitu unaona? Kuhesabiwa haki kwa imani, kutakaswa ,ubatizo wa Roho Mtakatifu; Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu kila kitu unaona?

Angalia, yeye alifanya nini katika kule kutoka kwa kwanza? Alitupa nabii aliyepakwa mafuta na nguzo ya moto, na akawaita watu watoke. huko ni kule kutoka kwake kwa kwanza. Na muda wa Israel ulipokwisha, alimtuma tena nabii Mungu pamoja na nguzo ya moto Yohana aliiona ikishuka kutoka mbinguni kama huwa (Yohana1:32-34) (Na Yeye Bwana Yesu Kristo) alisema nimetoka kwa Mungu na ninarudi kwa Mungu”(Yohana 16:28-30).huku kutoka kwa pili, alileta nabii aliyepakwa mafuta, ambaye alikuwa ni mwana wake, Mungu nabii. Musa alisema atakuwa nabii (Kumbukumbu 18:15-18)na alikuwa na nguzo ya moto na akafanya ishara na maajabu, na nabii yule yule alisema Yoyote aniaminiye mimi, kazi nizatendazo naye atazifanya (Yoh.14:12-13).

Na hapa ameahidi jambo lililile katika kutoka kwa siku za mwisho, na hawezi akalibadilisha hilo. Na kwa uthibitisho wa kisayansi, kwa ushuhuda wa Roho, kwa kazi za Roho tunalionga hilo leo, ile nguzo kuu ya moto ikitembea miongoni mwetu. Na ishara na maajabu ya kufufuka kwa Yesu Kristo kukiita watu kutoka kwenye udhehebu waje uweponi pa Yesu Kristo waishi; kwenda kwenye nchi.

Kule kutoka kwa kwanza, alifanya nini? Aliwatoa kutoka nchi ya asili kwenda nchi ya asili(Kutoka 12:37) kule kutoka kwa pili, aliwatoa wao kutoka hali ya kiroho na kuwaingiza katika ubatizo wa kiroho wa Roho Mtakatifu (Matendo 2:1-4). Sasa anawatoa wao kutoka ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, akiwaleta katika nchi ya milele ya utawala wa miaka elfu na yale makuu ya baadaye. Nguzo ile ile ya moto kwa utaratibu ule ule wa kupakwa mafuta, na Mungu yule yule akifanya mambo yale yale. [8]

Nenda katika kile chumba cha nabii na angalia zile hatua saba. Yule mlinzi alikabiliana na upinzani wapi wakati wa kumleta mgeni uweponi kwa mfalme si kule juu ya ngazi? Ilikuwa katika ngazi ya saba. Hapo inaonyesha kwamba inabidi tuje tena tuwe na Roho yule aliyekuwa ndani ya Yohana (Mbatizaji) alimtambulisha Mesiya; alikuwa mkuu kuliko manabii wote; alimtambulisha (Mathayo 11:7-11)

Na tumefika mahali tena, kwa kitu Fulani ambacho kitamtambulisha mesiya. Na wale watu ambao wanamwamini Yeye watamtambua, mpaka wawe kwenye neno wakati wote ili wamjue vile alivyo. Daniel alisema wenye hekima wataelewa, lakini wapumbavu, wote walio na hekima hawatajua (Danieli 12:9-10). Watamjua Mungu wao.

Sasa, jinsi alivyosema itatokea katika siku za mwisho ili kuwaleta watu wake tena kwenye Neno, ili kwamba Bibi arusi amjue Mume wake, amjue mpenzi wake, Neno lililofunuliwa. Ndiyo maana hilo lazima litokee. haikuwa wakati wa watengenezaji; haikuwa wakati wa Luther, Wesley na Wapentekoste na wote; maandiko yanasema haikuwa, lakini sasa itakuja; hiyo ni ahadi ya wakati huu.

Tunaishi wakati ambapo kuja kwake kutakuwa. Bibi aruri lazima atambulishwe na Yeye kila mwanamke lazima atambulishwe na mume wake, kwa maana hao wawili ni mmoja na Yeye ni neno, siyo dhehebu ni neno. Tunapaswa kuwa wana wa nuru (Yohana 12:36).na nuru ni neno. ambako nimefanywa nuru ya wakati. tutajuaje, nuru ila iwe kwenye neno. vema. lile neno limefanyika mwili ni nuru ya wakati unapoiona hiyo; Biblia ilisema hivyo [9]

Katika siku ya tatu (baada ya ufufuo) ndipo hasa udhihirisho wa Kristo ulipofanywa ujulikane, katika mwisho wa siku ya tatu.

Siyo katika siku ya kwanza; ilikuwa imekufa, katika siku ya pili ulikuwa bado umekufa; Luther, Wesley. mwanzoni mwa siku ya tatu kulikuwa na minong'ono. Hakukuwa na kitu katika siku ya kwanza (Luther), hakukuwa na kitu siku ya pili na katika siku ya tatu, (ule wakati wa Roho Mtakatifu) kulikuwa na minong'ono iliyoenea kuwa Yeye ni yule jana leo na hata milele. Lakini mwishoni mwa siku ya tatu ndipo alipojifanya mwenyewe ajulikane, alikuja hasa “kiongozi mwao, alikuja kati ya watu wake na kusema “niangalieni; ni mimi yule” (Luke 24:13-32).

Ile hali ya kufa iliendelea mpaka siku ya Pentecoste, ndipo ikaanza minong'o kuzunguka kwamba alikuwepo. Sasa wakati huu wa mwisho yuko hasa pamoja nasi, akitembea wazi miongoni mwetu.

Katika mwisho wa siku ya tatu. aliwatokea na kuwaonyesha wote ishara ya kufufuka kwake. Kwamba anaishi, kwamba alikuwa anaishi, Yeye ni yule jana, na leo na hata milele.

Matunda yaishio ya uwepo wake... matunda yaishio ya uwepo wake (mnalipatahilo?) yalidhihirishwa pale mwishoni kabisa wakati alipotokea kwa wale wote. kanisa lake.(Luka 24:36-46).Amen kwa nini? Wote walikusanyika pamoja oh. Amen. katika mwisho wa siku ya tatu.....unalipata hilo? Aamen. kwa maana Mungu alisema, nitawa "rudishia" (Joel 2:23-27). Ataenda kuwarudishia kwa namna gani? Kwa njia ya wajumbe wanne wa mauti waliliuwa hilo, halafu wajumbe wanne wa uzima wanalirudishia (Yoeli1:1-4). Ya kwanza ilikuwa nini? John Wesley...kwa utakaso. ya tatu ilikuwa nini? Pentecoste na kurudishiwa vipawa vya, Roho Mtakatifu ubatizo wa Roho Mtakatifu .yanne ilikuwa nini? lile neno. nini? lile neno.

Nuru ya nne itakuja ambayo italeta ishara zile zile. Angalia. kuhesabiwa haki kwa imani ilikurudisha ule utomvu kutakasiwa kulileta lile gamba: fundisho la utakatifu. nini kilileta tena lile jani? Wapentekoste. Kitu gani? Majani, yakipentecoste, kupiga makofi, furaha, kushangilia. Wapentecoste nini? Ya nne ilikuwa ni lile neno lenyewe. neno likiwa limefanyika mwili, thibitisho la tunda la ishara ya kufufuka kwamba Kristo hatimaye/mwishoni, baada ya kuhesabiwa haki tukiwa tumepandwa, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Madhehebu yamekufa na Kristo tayari tena amejikweka katikati pale kama kifuniko cha piramid.mstari wa kwanza, kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, halafu kinakuja kile kifuniko. Ni nini? Kundi lile la Roho Mtakatifu likichongwa. ilikwamba liweze kuungana na huduma ile ile. Aliyokuwa nayo alipoondoka, ili wakati anapokuja tena italipasa hili lote kuwa unyakuwo, ambapo ameshahesabiwa haki;wametakaswa, na kubatizwa na Roho Mtakatifu. Ile piramidi itakuja kusimama. Nyumba ya Mungu itaishi tena. Mti wa uzima unakuwa tena [10]

Sasa kumbuka kuwa Kristo amefufuka kutoka kwa wafu na yuko miongoni mwetu kati yetu.

Sasa tumeona aina kuu nyingi za uamsho, na kupiga kelele na kumsifu Mungu; yote ni mazuri. Tumenena kwa lugha na kutabiri, na vyote, tumeona haya yote, hilo ni zuri hayo yanakuja pamoja na hilo.

Lakini kumbuka, kitu cha mwisho ni uwepo Mungu, lile neno lenyewe,Yeye ni neno. kile kichwa, lile neno, linakuja katika mwili. unaona? na halafu lile neno, katika Waebrania sura ya nne (mstari 12-13)

,alisema,"neni la Mungu li hai, tena linanguvu, kuliko upanga ukatao kuwili tena ni jepesi kuyatambua mawazo na makusudio ya moyo" sasa chukuwa hayo maandiko na uyafulitilie kule nyuma tangu mwanzo wa manabii, yafuatilie mpaka wakati wa Yesu Kristo, na uone kama sio jambo lile, kwamba anajulikana kama Mesiya.

Sasa, sio mtu Fulani hapa aliye Mesiya, ni Roho Mtakatifu ndiye Mesiya, Kristo na Roho Mtakatifu ni jambo lililile, kwa hiyo hilo liko hapa sasa likitenda tu kupitia mwili kuuwekaa mwili tayari kwa ile neema ya kunyakuliwa liamini hilo marafiki. [11]

Kama tungetambua tu kuwa anatutokea sisi katika hii mikutano kwa kusudi moja, ambalo ni kutoa mahitaji yetu tulionayo kwake Yeye, lakini inabidi tutambue uwepo wake. Na sasa, kwa namna gani unavyotambua uwepo wake. ni wakati neno la ahadi lililodhihirishwa, siyo neno lililoahidiwa la Musa la wakati au wakati mwingine wowote, ahadi ya neno la wakati(Luaka 17:28-37;Ufunuo 10:1-11) [12]

Ni kwa hakika ninawaheshimu Walutheri kwa msimamo wao katika siku zao Wamethodist kwa utakaso katika siku zao na kwa Wapentecoste msimamo wao katika siku yao;lakini tunaishi katika siku nyingine, tunaishi wakati kumeshakuwepo na ubua, kuchanua, kapi, linafanana sana na ngano, lakini ngano iko ndani ya kapi. Lile kapi limeishikilia ngano, limeshifadhi isiunguzwe na jua kali, na sasa madhehebu yanajitenga nayo, ili iweze kukaa uweponi kwa mwana (son) ili uweze kuiva. Hakutakuwa na madhehebu tena ili huu ni mwisho wa hayo. Tunakuwa kila mara kama miaka mitatu, ujumbe ukianza wanaunda dhehebu

Hii imekuwepo ikiendelea karibu miaka ishirini na hakuna dhehebu haiwezekani .Tuko wakati wa ngano, wakati wa mavuno. Ninaweza kusikia ile mashine kuu ya kuvunia ikija. Tunaenda nyumbani siku moja. kweli"Yeye ni yule jana leo na hata milele [13]

Ninaamini tunao ukweli. Nimeridhishwa na hilo. na ninaamini ngano ni dhahiri ,makapi yanajitenga nayo.Llakini ngano inabidi ikae uweponi pa jua ili ikomae. Na tuko hapa kwa ajili yahilo, marafiki kaa uweponi kwa mwana mpaka makundi kidogo ya watu hapa, mpaka yawe yameiva kwa Kristo, kwamba yawe ni mkate mezani kwake. Hicho ndicho nitakachofanya. [14]

Nukuu za kiingereza:

[1]tangu wakati huo(62-0713),aya E-102

[2]kumfunua Mungu 64-0614m,Aaya 129-136,312

[3]Kristo aliye tambulishwa kwa nyakati zote(64-0617),Aya 42

[4]Kristo anatambulishwa ni yule yule(64-0415),Aaya

[5]Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa (63-0728),uk.70

[6]ile mbegu ya hitilafu(65-0118)Aya 126

[7]Muhuri wa pasaka(65-0410) uk 39

[8]kule kutoka kwa tatu(963-0630m)uk 40-45

[9]karamu ya baragumu(64-0719m) uk,17-18
[10]kurudishiwa mti wa bibi arusi(62-0422),uk 73-76
[11] Jehovajire (64-0402)aya 193-196
[12]uwepo wa Mungu uliotambuliwa (64-0618) Aya 76
[13] JeMungu hubadilisha mawazo yake (65-0427) Aya 213-214
[14]mtu anayejiiepusha na uso wa Bwana (65-0217).Aya 38

*jiwe la kiroho la kujengea na 173 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii,
iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany
(+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de*

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na
mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.
(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:

*Charles E. Y. Kanju,
Box 553 Korogwe - Tanga
E-mail: Chaelika@livel.com
Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*